# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**,

Naanza kwa kumshukuru Mwenyeenzi Mungu Mwingi wa Rehema na Muweza juu ya kila jambo ambaye anastahiki kushukuriwa kwa kunijaalia mimi pamoja nanyi pumzi na afya njema na zikatuwezesha kuwepo hapa muda huu kuwasilisha Hotuba hii, hivyo tukaweza kutimiza wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi sambamba na ujenzi wa Taifa letu.

Pia, nina wajibu wa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunigaiya muda wako nikaweza kusimama mbele ya hadhara hii ya Waheshimiwa wajumbe wa Baraza kuwasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba pia, kwa dhati ya moyo wangu nichukuwe nafasi hii kumshukuru na kumpongeza, Mheshmiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizu Dkt Ali Mohamed Shein.

Ni ukweli uliowazi na naamini kila mwenye tafakuri pana atakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Dkt Ali Mohamed Shein, ni Mtumishi na Kiongozi nambari moja, mzalendo, mkweli, aliyejaa busara, mweledi, asiye na majivuno mpenda maendeleo na anayemjali kila mmoja wetu. Namuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na maisha marefu, busara, hikima na afya njema ili tuweze kuendelea kuchota busara zake zaidi.

Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) kwa kuiongoza Ofisi hii muhimu kwani ndio inayotoa taswira inayomuakisi kiongozi wetu mkuu wa nchi. Vile vile nawapongeza watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu na watendaji wenzake kwa kazi nzuri wanazofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika,**

Katu sitaweza kunyanyua ulimi wangu kuendelea na hotuba hii pasi na kupeleka pongezi na shukurani za pekee kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Daktari Abdulhamid Yahya Mzee kwa umakini, busara na uhodari kwani yeye ndiye kiongozi wa watumishi wote na mtendaji mkuu katika Ofisi yetu ya Baraza la Mapinduzi, chombo ambacho ndio Dira na Mwelekeo wa nchi na kila mmoja wetu anakiamini na kukithamini sana. Mungu amjaalie afya njema na umri mrefu na aendelee kulitumikia Taifa kwa utumishi wake uliotukuka.

**Mheshimiwa Spika,**

Sasa naomba niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe na Makatibu wa Kamati kwa kazi nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza hili, kwa kuendelea kuwawakilisha vizuri wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Kusismamaia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Panya Ali Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Shihata) | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Viwe Khamis Abdalla | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Ame Haji Ali | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Rashid Ali juma | Mjumbe |
| 7. | Mheshimiwa Mtumwa Suleiman Makame | Mjumbe |

Aidha Kamati hii inafanyakazi na makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia na kutushauri ipasavyo katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yameipatia Kamati hii heshima na mafanikio makubwa. Makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Karima Abdul-Wahab | Katibu |
| 2. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Ni jukumu la Kamati kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Wizara. Katika kutekeleza hilo Kamati ilikaa na kujiadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 23/04/2020 na leo hii kwa niaba ya Kamati nawasilisha maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo naomba kuwasilisha maoni ya Kamati mbele ya Baraza lako kwa kuanzia na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imepanga bajeti yake kupitia mafungu (vote) mawili ambayo ni A01[1] na A02[2] yenye Programu Kuu Tano zilizobeba Programu Ndogo Kumi na Moja .

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla Fedha iliyoombwa kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni TZS. **9,563,500,000 (Bilioni Tisa, Milioni Mia Tano na Sitini na Tatu na Laki Tano)** na kwa upande wa Baraza la Mapinduzi ni TZS 2,**237,600,000 (Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili na Thelathini na Saba na laki Sita)**. Kwa ujumla fedha zinazohitajia kwa mwaka wa fedha **2020/2021** ni jumla ya TZS **11,801,100,000 (Bilioni Kumi na Moja, Milioni Mia Nane na Moja na Laki Moja)**

[1] **Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

[2] **Baraza la Mapinduzi**

**Mheshimiwa Spika,**

Fungu A01 ina jumla ya Programu Kuu tatu na Programu Ndogo Nane, Programu Kuu ni kama zifuatazo:

1. Programu ya kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha Mawasiliano Ikulu.
2. Programu ya kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nchi za Nje (Diaspora).
3. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha; Programu Ndogo za Programu Kuu hizo ni kama zifuatazo:

I. Programu ndogo ya kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais
II. Programu ndogo ya kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi
III. Programu ndogo ya kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda na kimataifa.
IV. Programu ndogo ya uratibu wa Shughili za Wazanzibar Wanaoishi Nje ya Nchi.
V. Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
VI. Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Mipango, Sera na utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
VII. Programu ndogo ya uratibu na usimamia wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi- Pemba
VIII. Programu ndogo ya usimamizi wa usalama wa watumishi wa Umma

**Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu.**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina Jukumu la kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais pamoja na kuimarisha Mawasiliano, ambayo ndani yake ina programu ndogo mbili; ya

kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na ya kuimarisha mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi. Programu Kuu hii imetengewa jumla shilingi **4,222,795,000 (Bilioni Nne, Milioni Mia Mbili na Ishirini na Mbili, laki Saba na Elfu Tisini na Tano)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeridhika na fedha zilizotengwa na ofisi kupitia programu kuu hiyo katika kuhakikisha kwamba Idara hizo zitaweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kama ilivyokuwa kwa mwaka wa fedha **2019/2020.**

Ni matumaini ya Kamati kuona kwamba fedha zilizoombwa kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** kuwa zitatumika kama zilivyokusudiwa na zitasaidia sana kuweka ukaribu baina ya wananchi na Serikali yao.

**Programu ya kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje (Diaspora)**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina lengo la kuiwezesha Zanzibar kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, na kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yao. Programu hii ina programu ndogo mbili ambazo ni programu ndogo ya kuiwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya kikanda na kimataifa ambayo imepangiwa kutekelezwa kwa shilingi TZS, **743,323,000 (Milioni Mia Saba na Arubaini na Tatu, Laki Tatu na Elfu Ishirini na Tatu)** ambapo miongoni mwa shughuli zilizopangwa ni pamoja kujenga uwelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na jumuiya za mtangamano wa kikanda (EAC, SADC na AU) na kujenga ushirikiano wa kimataifa. Kamati inashauri yale yote ya msingi yatakayojadiliwa katika Mikutano hiyo na yenye tija kwa Zanzibar ni vyema tukayazingatia na kuyatumia katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Programu Kuu hiyo, katika Program Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibar Wanaoishi Nje ya Nchi, ambapo kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** miongoni mwa majukumu ya Idara ni pamoja na kujenga uwelewa kwa jamii juu ya

Sera ya Diaspora Zanzibar na utekelezaji wake. Mbali na kuweka mazingira ya kujenga uwelewa kwa Sera ya Diaspora, Kamati inasisitiza kazi kama hiyo kufanywa pia kwa upande wa Sheria kwani kuwa na Sheria ni jambo moja na utekelezaji wake ni jambo jingine.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo Kamati inapongeza Idara kwa mpango huo waliojipangia na inasisitiza Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi kuwa na mipango endelevu katika kuwashajihisha Wanadiaspora kuzidi kusaidia katika utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi hasa katika kipindi hiki kigumu cha Janga la Maradhi ya **COVID 19** ambapo mchango na msaada wao unahitajika zaidi kwa ndugu zao walipo Zaznzibar**,** pamoja na kuwekeza katika miradi mbali mbali ya kiuchumi Zanzibar.

**Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ina malengo ya kuimarisha shughuli za mipango, kuandaa na kuchambua sera na utafiti pamoja na kuimarisha uwezo wa kiutendaji na uratibu wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Program Kuu hii ina programu ndogo nne ambazo ni programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa shughuli za Ofisi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Mipango Sera na Utafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Programu ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindizi Pemba na Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yenye lengo la kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imepangwa kutekelezwa kwa jumla ya shilingi za TZS **4,597.382,000**

**(Bilioni Nne, Milioni Mia Tano na Tisini na Saba, Laki Tatu na Themanini na Mbili Elfu)** ambazo zinakadiriwa kutumika katika shughuli za kusimamia uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa shughuli zilizopangwa katika Programu Kuu hiyo ni pamoja kutoa taaluma ya ufahamu juu ya maradhi yasiyoambukiza na umuhimu wa kupima afya zao. Kamati imeridhika na mpango huo wa kujua afya za watendaji wao, hata hivyo Kamati inashauri elimu hiyo yende sambamba na kuwapa taaluma juu ya kujikinga na Janga la Maradhi ya **COVID 19** kwani ni janga la kimataifa na kila mmoja wetu anapaswa kuchukua tahadhari ya hali ya juu ili kujikinga na maradhi hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuhusu suala la jengo kwa ajili ya Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO) nalo lipewe uzito unaostahiki kwani hivi sasa maafisa wa Ofisi hiyo wamekuwa wakifanya kazi katika Ofisi ndogo isiotosha kutokana na mahitaji yao.

Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Rais kuwapatia jengo Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO) ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi pamoja na kuwa katika mazingira yalio bora zaidi kulingana na majukumu yao.

Aidha, Kamati imeridhika kuona kwamba Wizara ina mpango wa kuanda Sheria ya Usalama wa Serikali GSO. Hivyo ni matumaini ya Kamati kuona kwamba Idara ya Usalama wa Serikali inapata Sheria nzuri na bora ambayo itawezesha Idara hiyo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni dhahir kwamba hatua waliyoichukua Wizara kwa mwaka wa fedha **2019/2020,** ya kuwasilisha Sheria ya Mambo ya Rais na Diaspora katika Baraza hili la Wawakilishi ambazo kwa sasa zipo tayari kwa ajili ya matumizi ni jambo la kupongezwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, kuhusu suala la kuanda mkutano wa kutunuku nishani, kwa kweli Kamati imefurahishwa kwani kukamilika kwa Sheria ya Mambo ya Rais ambayo imeweka

utaratibu mzuri wa kuongoza vikao hivyo kupitia Kamati zake za Ushauri na ya Sekritariati. Hivyo, Kamati inashauri Sheria hii ifuatwe ili mikutano hiyo iwe yenye ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM, Kamati imefarajika kuona kwamba katika mwaka wa fedha **2020/2021,** Wizara kuwa na mpango wa kufanya utafiti juu ya athari za mmon'gonyoko wa ardhi katika Nyumba za Ikulu pamoja na gharama za kudhibiti maeneo hayo ni jambo la kupongezwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilitarajia kuona kwamba kupitia Miradi ya Maendeleo ambayo kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** jumla ya shilingi za TZS **1,500,000,000,** zimepangwa kutumika na wizara katika miradi hiyo, ambapo miongoni mwa shughuli zilizopangwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Rais katika Ikulu ya Micheweni, kuzuia mmong'onyoko katika nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Rais katika Ikulu ya Migombani.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, Kamati inashauri Wizara kuchukua hatua ya dharura ya kudhibiti eneo la Ikulu ya Kibweni ambalo kwa sasa linaonekana kuwa na mmon'gonyoko mkubwa ambao unatishia usalama katika eneo hilo. Hivyo, ni vyema kuchukuliwa hatua za haraka ili kuweza kulinusuru eneo hilo, kama hatua zilizochukuliwa katika Ikulu ya Mkoni ambapo kwa sasa lipo katika hatua nzuri ya kulinusuru eneo hilo.

Kwa ujumla Programu Kuu hii imeweza kujikita katika programu ndogo nne ambazo kwa kweli katika mwaka wa fedha **2020/2021**, kupitia programu hii Wizara imeweza kupanga shughuli ambazo Kamati imeridhika nazo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu pia imepitia Fungu A02 Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ambalo ni Fungu linalojitegemea na kusimamiwa na Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la

Mapinduzi, Fungu hili lina Programu Kuu mbili na programu ndogo tatu, programu kuu hizo ni zifuatazo:

1. Programu Kuu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi
2. Programu Kuu ya Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi,

Kwa upande wa Programu Ndogo kama zifuatazo ni:-

i. Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na mjukumu ya KBLM/KMK
ii. Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma
iii. Programu ndogo ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia Programu Kuu na Progamu Ndogo katika Fungu hilo la A02 kwa mwaka wa fedha **2020/2021,** kwa Baraza la Mapinduzi imepanga kutumia jumla ya shilingi TZS **2,237,600,000** kwa kazi za kawaida.

**Mheshimiwa Spika,**

**Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi**

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya usimamizi wa Majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu ambayo ina lengo la kutayarisha na kusimamia vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu, programu hii ina Programu ndogo mbili, Programu ndogo ya kwanza ni Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na majukumu ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Programu ndogo Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Taasisi za Umma ambapo imekadiriwa kutekelezwa kwa TZS **805,480,000 (Milioni Mia Nane na Tano Laki Nne na Themanini Elfu)** kwa mwaka wa fedha **2020/2021.**

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa shughuli zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na kutayarisha Mikutano kati ya Mheshimiwa Rais na Wizara za SMZ, kutathmini utekelezaji wa Mipango kazi na kufuatilia utekelezaji wa maagizo na maelekezo yake, kutayarisha vikao vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yake pamoja na kufuatilia utekelezaji wa masuala maalum ya Sera, Sheria na Maamuzi ya Serikali, kupitia Programu ndogo hizo. Kamati imeridhika na mpango huo na inatarajia kuwepo kwa utekelezaji uliobora kwa maslahi ya nchi na jamii kwa ujumla.

**Programu ya Utumishi na Uendeshaji Ofisi ya Baraza la Mapinduzi**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Fungu A02, Kamati pia ilipitia Programu Kuu ya Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi yenye lengo la kuimarisha mazingira ya kazi, mahusiano ya umma na kuwaongezea ujuzi wafanyakazi wa Ofisi. Programu hii ina Programu ndogo mmoja ambayo ni Programu ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. kupitia Programu ndogo hiyo Ofisi imepangiwa kutekeleza shughuli zake ambazo miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kuimarisha huduma za maktaba na kitengo cha uandaaji, usambazaji na uhifadhi wa kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi ambapo kwa mwaka wa fedha **2020/2021**, jumla ya TZS **1,432,120,000 (Bilioni moja, Milioni Mia Nne na Thelathini na Mbili, Laki moja na elfu ishirini)** zinatarjiwa kutumika katika kutekelezwa shughuli mbali mbali, kupitia Programu Kuu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa Fedha **2020/2021**.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

……………………………….

Panya Ali Abdalla,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**